



## The translator's visibility in post-colonial context



Research Article



Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the **Research Journal in African Languages**, Volume 3, Issue 1, 2022

© 2022 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

### Article Information

Submitted: 15<sup>th</sup> December 2021

Accepted: 4<sup>th</sup> March 2022

Published: 11<sup>th</sup> March 2022

Additional information is available at the end of the article



<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

ISSN: 2709-4316 (Print)

ISSN: 2709-4324 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code



<sup>1</sup>Vincent N. Magugu, <sup>2</sup>Robert W. Oduori, <sup>3</sup>Mosol Kandagor

Department of Kiswahili and Other African Languages, Moi University, Kenya

Correspondence: [njeruwamagugu@gmail.com](mailto:njeruwamagugu@gmail.com)

 <https://orcid.org/0000-0002-6834-880X>

### Abstract

Developments within translation studies during the early nineteen nineties changed the perception of the concept translation into a dynamic and ever-expanding one. The expanded scope has redefined and reshaped the role of the translator from that of a passive and unbiased conduit from one language and culture to another. Concepts such as equivalence, faithfulness as well as translation quality, that henceforth were deemed to be central to translation studies have been relegated to peripheral status with extra-textual features taking center stage. The interpretation and translation of a text have since shifted from a purely linguistic and textual paradigm to a more encompassing extralinguistic and cultural one. This holds true for translated literature in postcolonial contexts. The translator is foregrounded through deliberate attempts to ensure that the translated text reads like a translation through foreignization strategies. These strategies align with the otherness that is characteristic of postcolonial contexts linguistically and culturally. By analyzing the translation of Ngugi wa Thiong'o's novel, *Devil on The Cross*, from Kikuyu, this paper discusses how the translated text has been modeled into a field of renegotiating colonial imperialist language and cultural positions. It further looks into the translator's visibility through his deliberate linguistic choices.

**Keywords:** foreignization, postcolonial translation, translator visibility



### How to Cite:


Magugu, V. N., Oduori, R. W., & Kandagor, M. (2022). Udhahirikaji wa mtafsiri katika muktadha wa baadaukoloni. *Research Journal in African Languages*, 3(1).

Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/744>





## Udhihirikaji wa mtafsiri katika muktadha wa baadaukoloni



Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the *Research Journal in African Languages*, Volume 3, Issue 1, 2022

© 2022 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

### Article Information

Submitted: 15<sup>th</sup> December 2021

Accepted: 4<sup>th</sup> March 2022

Published: 11<sup>th</sup> March 2022

Additional information is available at the end of the article



<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

ISSN: 2709-4316 (Print)

ISSN: 2709-4324 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code



<sup>1</sup>Vincent N. Magugu, <sup>2</sup>Robert W. Oduori, <sup>3</sup>Mosol Kandagor  
Department of Kiswahili and Other African Languages, Moi University, Kenya

Barua pepe: [njeruwamagugu@gmail.com](mailto:njeruwamagugu@gmail.com)

<https://orcid.org/0000-0002-6834-880X>

### Ikisiri

Maendeleo katika taaluma ya tafsiri mwanzoni mwa miaka ya tisini yalibadilisha mtazamo kuhusu dhana ya tafsiri na kutambua upana na mabadiliko yake. Kupanuka kwa upeo wa taaluma hii kumeeleza na kuumba upya dhima ya mtafsiri. Nafasi ya mtafsiri imebadilika kutoka kwa daraja la kuvusha ujumbe pasi kuuathiri hadi kumtambua mtafsiri kuwa kiungo muhimu kinachoathiri mchakato na zao la tafsiri. Dhana kama vile ulinganifu, uaminifu pamoja na uhakiki wa ubora ambazo awali zilikuwa zenye umuhimu mkuu katika taaluma ya tafsiri zimesukumwa pembeni huku vipengele visivyokuwa vya kiisimu vikitiliwa mkazo. Ufasili na utafsiri wa matini ambao awali ulikuwa mchakato wa kiisimu na kimatini umebadilika na kujiegemeza zaidi kwa vipengele vya kitamaduni na vipengele nje ya isimu. Hali hii ni kweli tunapodhukuru tafsiri za fasihi katika muktadha wa baadaukoloni. Mtafsiri anadhihirika bayana kupitia kwa uteuzi wa kimakusudi ambao unajiegemeza kwa mikakati ya uibuaji ugeni hasa katika kushughulikia vipengele vinavyofungamana na utamaduni chanzi. Mikakati hii inaibuwa lugha mesto ambayo inahusiana kwa karibu na dhana ya utofauti wa kiisimu na kitamaduni katika mazingira ya baadaukoloni. Kwa kuchunguza tafsiri ya riwaya ya Caitani Mutharaba-ini ya Ngugi wa Thiong'o kwa Kiingereza, Makala hii imejadili jinsi matini tafsiri imegeuzwa kuwa jukwaa la kukabiliana na ubabe wa kibepari katika ngazi ya isimu na utamaduni pamoja na jinsi udhihirikaji wa mtafsiri unavyobainika kupitia kwa kuchunguza uteuzi wa kimakusudi wa kiisimu ambao mtafsiri alifanya.

**Maneno Muhimu:** uibuaji ugeni, tafsiri za baadaukoloni, udhihirikaji wa mtafsiri



### How to Cite:

Magugu, V. N., Oduori, R. W., & Kandagor, M. (2022). Udhihirikaji wa mtafsiri katika muktadha wa baadaukoloni. *Research Journal in African Languages*, 3(1). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/744>



## Utangulizi

Taaluma ya tafsiri, kama ilivyo kwa fani nyingine za usomi, imekua na kubadilika kadri ya mpito wa maisha. Taaluma hii kama uwanja maalum wa usomi iliimarika pakubwa hasa katika karne ya ishirini kinadharia na kiutafiti. Miongoni mwa michango muhimu iliyotokea katika karne hii ya ishirini ni pamoja na mchango wa Holmes (1972) ambaye katika ramani yake ya tafisi, zaidi ya kuipa taaluma ya tafsiri kitambulisho rasmi, alibainisha upeo wa taaluma hii na kuweka bayana maeneo anuwai ya kushughulikiwa katika usomi na utafiti wa tafsiri. Mojawapo wa maeneo aliyobainisha kama tawi la taaluma ya tafsiri ni uhakiki wa tafsiri mbalimbali.

Mawazo haya ya Holmes yamekuwa msingi kwa watalamu wa tafsiri wa baadaye ambao wamezidi kupanua upeo wa ramani aliyoipendekeza ili kuweza kuakisi uhalisia wa sasa wa utafiti na usomi katika tafsiri. Toury (1985) anaisifu ramani hii na kueleza kwamba ilikusudia kuweka msingi wa taaluma kamili ya kisayansi. Msingi huu unadhihirika tunapoangazia kwa mfano Williams na Chesterman (2002) ambao katika kitabu chao *The Map: A beginner's guide to doing research in translation studies*, wanatumia istilahi za kimsingi pamoja na baadhi ya mihimili aliyobainisha Holmes kama vile anwani ya taaluma ya tafsiri pamoja na tanzu za taaluma hii. Upeo wa maeneno ya utafiti ambao wameangazia katika kitabu hiki, japo umetoa taarifa za utondoti, pakubwa umejikita kwa upeo mpana uliobainishwa katika ramani ya Holmes.

Tunapotalii taaluma ya tafsiri kimapokeo, inabainika kwamba uhakiki wa tafsiri kwa kiasi kikubwa ulijikita katika uchanganuzi linganifu wa vipengele vya kiisimu, hasa vya kisemantiki, baina ya matini chanzi na matini tafsiri. Hali hii inadhihirika tunapochunguza mielekeo ya kinadharia kama vile nadharia ya ulinganifu wa kiisimu ya Catford (1965) ambapo anahimiza haja ya nadharia yoyote ya tafsiri kujikita katika vipengele vya usayansi wa lugha. Hata hivyo, katika awamu hii pia, paliibuka watalamu kama vile Nida (1964) ambaye licha ya kutambua umuhimu wa isimu katika tafsiri, alibainisha kwamba pana haja ya kuzingatia ulinganifu katika ngazi ya kimawasiliano. Utambuzi huu ulikuwa hatua muhimu ambayo iliweka msingi wa kupanua mielekeo ya kuhakiki tafsiri kinyume na kuzingatia vipengele vya kiisimu pekee. Hii ndio maana utafiti wa maendeleo katika taaluma ya tafsiri, hasa kuanzia mwishoni mwa miaka ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini, unadhihirisha kuwa msisitizo katika uhakiki wa tafsiri unaelekezwa kwa vipengele visivyo vya kiisimu. Kwa mfano, kufikia mwishoni mwa karne ya ishirini, paliibuka wataalamu walioandama mtazamo wa kiuamilifu hasa wasomi wa kijerumani kama vile Reiss na Vermeer (1984) na Nord (1997) kupitia kwa mapendekezo ya kinadharia almaarufu *Skopstheorie*. Wataalamu wanaoandama mielekeo ya kiuamilifu na kiuchanganuzi makinifu katika tafsiri wanahoji kuwa, kwa sasa hatuwezi kutafitia tafsiri pasi na kujumuisha vipengele vya kijamii, kitamaduni pamoja na muktadha kwa ujumla unaozalisha MC na MT.

Kupanuliwa kwa vipengele vya kuhakikiwa pamoja na mielekeo ya kinadharia katika uchanganuzi wa tafsiri kumeipanua taaluma ya tafsiri pakubwa. Licha ya hivyo, kupanuka huku kumeangaziwa zaidi katika mataifa ya kaskazini mwa ulimwengu na wasomi kama vile Venuti (1995), Tymoczko na Gentzler (2002), Cronin (2003, 2006) na Snell-Hornby (2006) miongoni mwa wengine kuliko ilivyo kwa mataifa ya kusini mwa uliwengu. Barani Afrika hata hivyo, kumekuwa na juhudi za kutafitia vipengele mbalimbali kama inavyodhihirika kutokana na kazi za wasomi kama vile Marais (2014, 2018) ambaye amezamia mwelekeo wa kisemiotiki katika tafsiri pamoja na Bandia (2008, 2010, 2014) ambaye amezamia suala la baadaukoloni katika

tafsiri na fasihi ya Afrika miongoni mwa wengine. Nchini Kenya, tafiti zimeanza kuendeshwa kuambatana na upeo mpya katika taaluma ya tafsiri na wasomi tofauti. Mfano bora kwa mwelekeo huu nchini Kenya ni utafiti wa uzamifu wa Zaja (2010) ambaye aliangazia tafsiri ya fasihi ya Kiswahili kwa kujikita kwa uamilifu wa vipengele vya muktadha na utamaduni.

Wananadharia katika taaluma ya tafsiri katika juhudi za kuendeleza taaluma ya tafsiri kinadharia na kiupeo wamezidi kuibuka na ramani mbalimbali zilizoimarishwa na zinazolenga kueleza upeo na kiini cha taaluma ya tafsiri. Miongoni mwa maendeleo muhimu katika taaluma ya tafsiri ni kubainishwa kwa mielekeo ya mwingiliano-taaluma hasa katika kutalii mielekeo ya kinadharia baina ya taaluma ya tafsiri na taaluma nyinginezo. Tafiti za tafsiri katika miaka ya karibuni zimevuka misingi ya kiisimu iliyosisitizwa na wasomi mwanzoni mwa karne ya ishirini na kuingia katika awamu muhimu inayopanua sio tu upeo wa kitaaluma bali pia kuibua namna mbadala za kuitafakari na kuangazia dhana ya tafsiri, mtafsiri, uamilifu wa tafsiri na wa mtafsiri pamoja na dhima ya tafsiri na ile ya mtafsiri katika jamii ya kisasa. Venuti (1995, 2008) kwa mfano anahoji kwamba, kwa muda mrefu msingi wa kutathmini tafsiri nzuri umekuwa ni ufasaha wa matini tafsiri kiasi kwamba inasomeka kama matini chanzi katika lugha lengwa. Hii ina maana kwamba, mtafsiri anakuwa kiungo ambacho hakina athari kwa mchakato wa tafsiri na kwa matini tafsiri. Anatazama kama kivukio tu ambacho hakiathiri mzigo au bidhaa inayovushwa. Mtazamo huu katika makala hii tunahoji kwamba ni jambo ambalo linakosa kutambua nafasi na athari ya kiungo hiki ambacho kimo katikati mwa mchakato mzima wa tafsiri. Tunakubaliana na maelezo ya Venuti (kshj) kuwa mtafsiri daima ana nafasi na athari katika uzalishaji wa matini tafsiri iwe ni nathari, ushairi au hata matini zisizo za kifasihi. Tukitumia mfano wa mpishi ambaye anaonjeshwa chakula kilichoandaliwa na mtu mwingine, kisha anatwikwa jukumu la kutumia viungo vilivyotumika kuandaa chakula alichoonjeshwa kuandaa mlo sawa. Jukumu la mpishi huyu wa pili ni changamano na linahusisha kuviweka viungo vyote pamoja kwa ustadi huku akipima na kufanya maamuzi kuhusu kiasi cha viungo, muda wa upishi na kadhalika ndipo aweze kuibuka na mlo wa kuvutia. Katika hali kama hii, ni vigumu kumtenganisha mpishi huyu na mlo anaandaa. Mlo wake utaathiriwa sio tu na viungo alivyopewa bali muhimu zaidi ni maamuzi anayoyafanya kimakusudi katika maandalizi yake. Vivyo hivyo, mtafsiri katika kuzalisha matini tafsiri anafanya maamuzi ambayo hatuwezi kupuuzwa iwapo tunahakiki zao la mchakato mzima wa tafsiri.

Tukiangazia maendeleo katika taaluma ya tafsiri, mojawapo wa vipengele vya kimsingi katika uhakiki wa tafsiri imekuwa ni dhana ya ulinganifu. Japo dhana hii ingali muhimu, mielekeo ya kuishughulikia na kuichunguza imebadilika na kupanuka. Aidha ulinganifu ulivyodhukuriwa kimapokeo hauzingatiwi tena kuwa ndio uti wa mgongo wa nadharia, taaluma na utekelezaji wa tafsiri. Ulingaisho wa kiisimu baina ya matini tafsiri na matini chanzi sio tena kigezo cha kipekee cha kushughulikia uhakiki wa tafsiri. Mitazamo inayotumiwa sasa katika kushughulikia dhana ya ulinganifu katika tafsiri imebadilika kutoka kwa maelezo yanayojikita kwa dhana za kiisimu na kwa sasa, ulinganifu unaangaziwa kwa njia pana inayojumuisha aina ya matini, muktadha pamoja na matumizi kama anavyoeleza Baker (1992).

Taaluma ya tafsiri ikiwemo tafiti katika uwanja huu zinaangazia masuala anuwai ambayo yamezidi kupanuka na kubadilika. Mabadiliko haya yameshika kani hasa baada ya mageuzi yaliyopinga msisitizo wa kuitazama matini tafsiri kama kimelea cha matini, na badala yake kuipa hadhi yake kama zao la michakato mbalimbali ikiwemo; mageuzi, ubunifu na uandishi upya

(Lefevere na Baker, 1992). Tafiti zimeangazia dhana anuwai zinazoathiri tafsiri na kudhihirika kupitia kwa tafsiri. Kwa mfano, Alvarez na Vidal (1996) katika kujadili tafsiri kama tendo la kisiasa anaeleza kuwa kinyume na mielekeo ya awali ambapo mtafsiri alikuwa "amefungwa" na matini chanzi, maendeleo ya kitaaluma yamedhihirisha kuwa mtafsiri ana uhuru wa kuifinyanga matini hii ili iafiki mfumo fulani wa imani na matarajio ya hadhira lengwa na utamaduni pokezi. Mageuzi yanayotokea yanaathiriwa na vipengele vinavyovuka sifa za matini chanzi na lugha chanzi na kujumuisha dhana zilizo nje ya upeo wa isimu kama vile upendeleo wa kiitikadi, mahusiano ya kiuwezo yanayojengeka, matarajio ya kitamaduni pamoja na uamilifu uliokusudiwa wa tafsiri husika. Mageuzi haya yanazalisha matini tafsiri ambayo inabainika moja kwa moja kuwa ni tafsiri na kwa jinsi hiyo inadhihirisha nafasi na dhima ya mtafsiri moja kwa moja.

Katika usanjari huu wa kuendeleza taaluma ya tafsiri kiupeo na kupanua kongoo ya tafiti zilizoendeshwa hasa katika mazingira ya bara la Afrika. Kiini cha Makala hii ni suala la udhihirikaji wa mtafsiri na dhima yake katika mchakato mzima wa tafsiri. Katika kutekeleza azma hii, utalii wa udhihirikaji huu umechanganuliwa kwa kujikita katika jinsi mtafsiri wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* kwa Kiingereza anavyodhihirika kutokana na jinsi alivyoshughulikia vipengele vya kitamaduni katika tafsiri yake.

### **Caitaani Mutharaba-ini and Devil on The Cross**

*Caitaani Mutharaba-ini* ni riwaya ambayo iliandikwa na Ngugi wa Thiong'o na kuchapishwa mnamo 1980. Kama anavyoeleza mwandishi, kwanza aliiandika kwenye karatasi shashi akiwa jela na katika lugha ya Kikuyu. Riwaya hii inaangazia matatizo ya kisiasa na kijamii yanayomkumba mwanachi wa Kenya wakati ule. Riwaya hii ni mojawapo wa riwaya maarufu zaidi za Ngugi wa Thiong'o japo umaarufu wake zaidi unatokana na tafsiri ya Kiingereza; *Devil on the Cross*. Ingawa riwaya hii ilitungwa kwa lugha ya Kikuyu, wahakiki kama vile Cook na Okenimpe (1997) wanaeleza kwamba ilikuwa na ukomavu wa kimaudhui na kintindo kuambatana na riwaya za awali ambazo Ngugi wa Thiong'o alikuwa ameziandika kwa Kiingereza. Kama ilivyo kwa riwaya nyingine za Kiafrika, riwaya hii ilitumia mandhari ya Kiafrika pamoja na fasihi simulizi ya Kiafrika katika uwasilishaji wake. Riwaya hii imetumia dhana zinazofungamana na utamaduni wa jamii ya Wakikuyu pamoja na jazanda zinazofasirika tu katika muktadha wa utamaduni huu. Maudhui ya riwaya hii ni mazito japo yanawasilishwa kwa mtindo wa kinaya ambapo wezi wanashindana na kueleza hila zao hadharani. Wageni waheshimiwa ni wezi kutoka muungano wa wezi wa kimataifa. Mtindo uliotumiwa katika kuiandika riwaya hii, hasa matumizi ya lugha, unasheni vipengele vya fasihi simulizi ya Wakikuyu ikiwemo matumizi ya nyimbo, mashairi, balagha, misemo na methali. Uteuzi huu ulichukuliwa kuwa wa kimakusudi na unaoeleweka kwa kueleza matini hii katika muktadha wake wa kihistoria. Uhawilishaji na uwakilishi wa dhana hizi katika tafsiri ya Kiingereza uliangazia kama msingi wa ubainishaji wa udhihirikaji wa mtafsiri.

### **Tafsiri ya Kiingereza - Riwaya ya Devil on the Cross**

Riwaya tafsiri ya *Devil on The Cross*, sio zao la mchakato wa tafsiri pekee ila inabainishwa kuwa inasheni vichocheo vya kitamaduni na kiitikadi ambavyo vilimpa mtafsiri msukumo wa kutekeleza. Hii ni tafsiri-binafsi iliyochapishwa mnamo 1982. Katika muktadha wa tafsiri hii,



mwandishi ndiye mtafsiri hivyo inatazamiwa kwamba anaelewa vyema lengo la matini chanzi. Hata hivyo, kuna uwezekano kwamba malengo ya matini tafsiri yanafanana au hata kutofautiana na yale ya maini chanzi jambo ambalo linaathiri mikakati na mbinu zilizotumika katika tafsiri hii.

Uwezekano wa tofauti za malengo baina ya matni chanzi na matini tafsiri unahusishwa na masuala kama vile hadhira inayolengwa. Tofauti kama hizi aiddha zinazoweza kusababishwa na vipengele zaidi ya utamaduni wa hadhira lengwa na badala yake vikahusishwa na imani na itikadi ya mtafsiri pamoja na uchanganuzi wa lengo la tafsiri yenyewe. Utambuzi wa mtafsiri kama kiungo ambacho kinaweza kuathiri tafsiri, mchakato pamoja na zao ni muhimu katika kutalii ushirikaji wake. Maoni haya yanashadidiwa na Reiss (1971) anavyonukuliwa katika Nord (1997) kwamba utokeaji wa ukosefu wa ulinganifu katika tafsiri wakati mwingine unatokana na michakato ya kimakusudi kama vile, wakati ambapo tafsiri inalenga kufikia lengo na uamilifu tofauti na matini chanzi. Anazidi kueleza kwamba tofauti pia zinaweza kutokea katika hali ambapo matini tafsiri inalenga hadhira tofauti na ile ya matini chanzi.

Katika makala hii, inabainika kwamba riwaya chanzi na riwaya tafsiri zilidhihirisha tofauti katika ngazi ya tafsiri hasa katika kigezo cha uibuaji wa athari sawa kwa kujikita kwa dhana za kitamaduni na zinazofungamana na utamaduni. Hali hii ilichukuliwa kuwa ilizalishwa na, miongoni mwa vichocheo vingine, juhudi za kimakusudi zilizoongozwa na uamilifu wa tafsiri zilizotekelezwa pamoja na kuathiriwa na mtafsiri mwenyewe. Tofauti hizi zimeangaziwa kuwa msingi wa udhihirikaji wa mtafsiri katika makala hii.

### **Udhihirikaji wa mtafsiri katika tafsiri ya *Caitani Mutharaba-ini* kwa Kiingereza**

Venuti (1995, 2008) katika kujadili suala la kudhihirika na kutodhihirika kwa mtafsiri anaibua dhana mbili ambazo ndizo msingi wa makala hii. Dhana ya kwanza ni ile ya ubinafsishaji na ya pili ikiwa dhana ya uibuaji ugeni. Kwa msingi wake, dhana hizi mbili zinaashiria mitazamo ya kimaadili miongoni mwa watafsiri kwa matini na utamaduni wa kigeni. Hizi ni dhana ambazo zinatokana na uteuzi wa matini ya kutafsiriwa pamoja na uteuzi wa mikakati inayotumiwa katika kuitafsiri matini husika. Ni muhimu kutambua kwamba, hakuna mpaka bayana baina ya ubinafsishaji na uibuaji wa ugeni. Hata hivyo, tunaweza kuzitofautisha dhana hizi kwa kuangazia maana yake. Kwa upande mmoja, ubinafsishaji ni dhana ambayo inahusishwa na juhudi za kuhakikisha kuna uasilia katika matini tafsiri ambapo dhana za kigeni huumbwa upya ili kuafikiana na matarajio na desturi katika muktadha wa utamaduni lengwa. Kwa upande wa pili, uibuaji ugeni ni dhana ambayo inahusishwa na juhudi za upinzani ambapo dhana za kigeni huhawilishwa kwa njia ambayo inadhihirisha bayana kwamba matini tafsiri ina msingi wake katika utamaduni mwingine. Kwa kutumia mojawapo kati ya mikakati hii, mtafsiri aghalabu huwa ametekeleza uamuzi wa kimakusudi unaochochewa na dhima ya tafsiri pamoja na msimamo wa mtafsiri mwenyewe.

Katika kuchunguza tafsiri iliyotekelezwa ili kuzalisha riwaya ya *Devil on the Cross* kutoka Kikuyu, inabainika kwamba, kwa jumla mtafsiri alipendelea zaidi mikakati wa uibuaji ugeni katika kushughulikia tafsiri hii, hasa vipengele vinavyofungamana na utamaduni chanzi. Hali hii tumeinasibisha na dhima ya matini tafsiri ambayo ililenga hadhira tofauti na ile ya matini chanzi. Aidha, tumeihusisha na imani na msimamo wa mtafsiri kuhusu suala la lugha na utamaduni hasa mahusiano baina ya lugha na tamaduni za jamii zilizowahi kutawaliwa dhidi ya lugha na tamaduni za kibepari. Suala la msimamo wa mtafsiri amelijadili binafsi katika

machapisho yake; *Decolonizing the Mind na Detained: A Writer's Prison Diary*. Isitoshe, msimamo wake umejadiliwa kwa kina na wahakiki mbalimbali tangu miaka ya themanini.

Tukiangazia mifano ya baadhi ya tafsiri zilizotekelezwa kwa dhana zinazofungamana na utamaduni, tunapata kuna usharabu kutoka kwa fasihi simulizi ya jamii ya Wakikuyu hasa mtindo wa ufunguzi tukirejelea vitendawili kama inavyojitokeza hapa chini:

**Matini Chanzi:**

Ndaathii uu Ndathii uu! Muturi akiuga  
 Njira cia ategi. Wangari akiugira Wariinga  
 Aaca!  
 Oya kigacwa  
 Njira cia aturi! Gwata riingi!  
 Ndaagwata  
 Ndathii uu ndaathii uu!  
 Njira cia aturi  
 Aaca. Reehe kigacwa  
 Oya  
 Njira cia aruti-a-wira. Gwata o riingi  
 Ndaagwata  
 Ndaathii uu ndaathii ndoreete gwa ituika  
 Njira cia aruti-a-wira  
 Ii na aaca. Reehe kigacwa na ndigukugaca muno ni wamenya menya  
 Oya  
 Njira cia aregi...na no cio cia aruti-a -wira... (Ukurasa wa 67)

**Matini Tafsiri:**

"I walk this way and that way!" Muturi said.  
 "The ways of hunters." Wangari answered for wariinga.  
 "No!"  
 "Take a forfeit!"  
 "The paths of builders! Answer another riddle!"  
 "I walk this way and that way!"  
 "The path of builders."  
 "No. Give me a forfeit." It's yours."  
 "The paths of workers. Answer another." "I will."  
 "I walk this way and that way towards a revolution"  
 "The paths of workers."  
 "Yes and no. You owe me a forfeit, but I won't take everything, for you got half the answer." "I accept that"  
 "The answer is the paths of resistance...and those are the paths made by workers."  
 (Ukurasa wa 68-69)

Katika mfano huu, mwandishi wa MC amechota kutokana na dafina ya fasihi simulizi hususan kipera cha vitendawili miongoni mwa jamii ya Wakikuyu na kutumia mtindo wake katika matini chanzi. Kwa kufanya hivi, mwandishi anafanikiwa kuipa matini hii uasilia zaidi kwa hadhira yake kwa kuipa ladha ya kiasili katika jamii ya Wakikuyu. Hali hii inafikiana na mawazo ya Okara (1963) kwamba waandishi wa mataifa yaliyowahi kutawaliwa, hususan Afrika, aghalabu hujihusisha katika zoezi la kuandika fasihi simulizi yao kila wanapoandika fasihi hasa kimtindo na kwa kutegemea zaidi fasihi simulizi ya jamii zao. Matumizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika katika uandishi wa fasihi ya baadaukoloni yanatokana na maamuzi ambayo pakubwa huchochewa na misimamo ya kiitikadi. Watunzi kupitia kwa uandishi wa fasihi wanatumia vipawa vyao kuupa utamaduni wao asili; ambao awali ulichukuliwa kuwa duni, hadhi sawa na utamaduni wa mkoloni ambao awali ulichukuliwa kuwa babe na wenye hadhi zaidi. Juhudi kama hizi za kimakusudi ni sehemu ya juhudi pana za kutafuta kujikomboa kutokana na ubepari wa kiisimu na kitamaduni.

Mfano huu unasheheni diskosi ambayo ni ya kipekee katika utamaduni chanzi wa Wakikuyu ambapo usemaji wa kutumia mafumbo na vitendawili ni dhihirisho la busara na ufasaha au ukomavu katika mawasiliano. Mtindo huu kama anavyoeleza Bandia (2003) unaipa matini hii uasilia ambao hata unapotafsiriwa bado utasheheni vipengele vya utamaduni chanzi. Tukiangazia jinsi mtindo huu wa kutoa vitendawili ulivyotafsiriwa kwa Kiingereza, inabainika kuwa mtafsiri amedumisha uaminifu kwa mtindo asilia katika lugha ya Kikuyu na kwa jinsi hiyo, mtindo unaodhihirika katika matini tafsiri ni zao la uibuaji wa ugeni ambapo matini tafsiri inakosa uasilia katika mfumo wa lugha na utamaduni lengwa. Kutokana na uteuzi huu, MT inakosa uasilia moja kwa moja na kudokeza kwamba matini hii ina asili yake katika utamaduni tofauti. Kupitia ugeni huu, athari ya mtafsiri, nafasi yake na hata mchakato wa tafsiri unadhihirika bayana.

Hali sawa inabainika tunapoangazia maneno ambayo yanafungamana na utamaduni chanzi ambapo mtafsiri aliyadumisha moja kwa moja jinsi yalivyo bila juhudi za kuyaumba upya ili yaafikiane na mfumo pokezi wa Kiingereza.

**Matini Chanzi:**

Gicaandi (ukurasa wa 1)

**Matini Tafsiri:**

Gicaandi (ukurasa wa 1)

*Gicaandi* kwa upande mmoja ni dhana inayotumiwa kurejela kipera cha fasihi simulizi katika jamii ya Wakikuyu kinachoakisi kilele cha ulumbi na balagha katika jamii hii. Aghalabu husheheni mafumbo na huwasilishwa kwa mtindo wa majibizano kama ilivyo kwa ngojera. Wahusika, ambao huitwa waimbaji, hufumbiana mafumbo hadi wakati ambapo mmoja wao atashindwa kufumbua fumbo lililopo na hivyo mshindi kupatikana. Kwa kawaida uiambaji wa gicaandi huwa mrefu wenye beti zaidi ya mia moja hamsini kwa kutegemea umahiri wa waimbaji. Kwa upande mwingine, neno gicaandi linarejelea aina ya ala inayotumiwa katika utendaji/uimbaji.



Tunapoangazia jinsi neno hili limeshughulikiwa katika Matini Tafsiri, tunapata kwamba mtafsiri alihamisha dhana ya gicaandi moja kwa moja kutoka matini chanzi hadi Kiingereza. Hali hii ni dhahirisho la uibuaji ugeni ambapo dhana ya kigeni inaingizwa katika lugha nyingine na hivyo kuashiria bayana kwamba matini inayorejelewa sio asilia katika utamaduni husika. Uibuaji huu wa ugeni ni dhahirisho la uteuzi wa kimakusudi wa mtafsiri wa kuheshimu kipengele hiki cha kitamaduni katika matini chanzi na kuipa matini tafsiri ladha ya kigeni. Uteuzi huu unaafikiana na maelezo anayotoa Venuti (1995, 2008) kuhusu uhusiano wa mkakati wa uibuaji ugeni na juhudi za upinzani. Upinzani huu unapata uamilifu zaidi hasa tunapoziangazia matini zilizochunguzwa katika muktadha wa baadaukoloni ambapo tafsiri inakuwa jukwaa la kuumba upya mahusiano ya kiuwezo baina ya lugha na utamaduni wa mtawaliwa dhidi ya lugha na utamaduni wa kibepari.

Maamuzi ya kuteua maneno yanayofungamana na utamaduni chanzi na kuyahamisha jinsi yalivyo katika tafsiri katika muktadha huu yanabainika kuwa ni ya lazima na ya kimakusudi. Ya lazima kwa sababu dhana hii haina kisawe linganifu katika utamaduni lengwa kwa jinsi ambavyo fani ya uimbaji gicaandi inavyodhahirika katika utamaduni wa Wakikuyu. Hivyo basi, kando na dhima na msimamo wa mtafsiri, ukosefu wa istilahi faafu kufumbata ujumbe wa dhana iliyotumiwa katika matini chanzi unakuwa kichocheo cha uibuaji wa ugeni. Uteuzi huu aidha unabainika kuwa wa kimakusudi kwa kuwa mwandishi aliye pia mtafsiri anafahamu fika upana wa maana ya dhana hii katika muktadha wa matumizi kwenye riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na kwa jinsi hiyo hana budi kuidumisha katika matini yake. Uamuzi huu unajikita kwa mtafsiri mwenyewe na hivyo unabainika kuwa kiungo chenye uwezo wa kuathiri mchakato wa tafsiri na kuiathiri matini tafsiri.

Kwa kweli, tafsiri ya *Caitaani Mutharaba-ini* kwa Kiingereza imeegemea zaidi kwenye uibuaji wa ugeni ambao umemdhahirisha mtafsiri moja kwa moja na kuifanya matini tafsiri kukosa uasilia katika mfumo pokezi kinyume na ilivyokuwa desturi katika mielekeo ya kimapokeo katika tafsiri. Ukosefu huu wa uasilia katika mazingira ya baadaukoloni pia ni dhahirisho la upinzani ambao unatia najisi “utukufu” wa lugha na utamaduni wa kibepari.

Hali sawa inajitokeza katika kushughulikia majina ya wahusika ambayo ni ya kimajazi ambapo mtafsiri ameyawasilisha ifuatavyo:

**Matini Chanzi:** Robin Mwaura (Ukurasa wa 31)

**Matini Tafsiri:** Robin Mwaura (Ukurasa wa 32)

**Matini Chanzi:** Gitutu wa Gataanguru (Ukurasa wa 95)

**Matini Tafsiri:** Gitutu wa Gataanguru (Ukurasa wa 97)

**Matini Chanzi:** Kihaahu wa Gatheeca (Ukurasa wa 105)

**Matini Tafsiri:** Kihaahu wa Gatheeca (Ukurasa wa 107)

**Matini Chanzi:** Mwireri wa Mukiraa (Ukurasa wa 159)

**Matini Tafsiri:** Mwireri wa Mukiraa (Ukurasa wa 162)

**Matini Chanzi:** Nditika wa Nguunji (Ukurasa wa 176)

**Matini Tafsiri:** Nditika wa Nguunji (Ukurasa wa 178)

Majina ya wahusika hawa wote yanatokana moja kwa moja na sifa zao au maumbile yao kama yanavyoelezewa kwenye riwaya. Robin Mwaura ambaye ni dereva wa matatu ambamo matukio ya awamu ya kwanza ya riwaya yanatokea anabainika baadaye kuwa ni tapeli na mwizi. Anaweka pesa mbele ya utu kama inavyobainika Wangari anapoeleza kuwa hana nauli. Tukiangazia jina lake, la kwanza *Robin* linakaribiana kimatamshi na neno *Robbing* kwa Kiingereza ambalo linarejelea hali ya kuiba kwa kutumia mabavu. Jina la pili *Mwaura* tunaweza kulihusisha na kitenzi cha Kikuyu *Kwaura* ambacho katika lugha isiyo rasmi kina maana ya kuiba.

Gitutu wa Gataanguru ni jina la kimajazi ambalo linaunganisha majina mawili: *Gitutu* ambalo lina maana ya *funza mkubwa* na jina *Gataanguru* ambalo lina maana ya *Minyoo* katika hali ya udogo. Funza na minyoo ni vimelea na hunyonya wanyama wengine. Hii ni sifa ambayo inadhihirika katika ushuhuda anaotoa. Inabainika kwamba yeye amepata utajiri kwa kuwanyanya wafanyakazi; kuwanyonya damu na jasho lao, kama kimelea. Mwandishi zaidi ya kutumia majazi katika jina la muhusika huyu, anatumia utamaduni chanzi katika kuendeleza jina ambapo anatumia jina la mzazi kama ilivyo kaida katika jamii ya Wakikuyu. Kwa mfano, mwandishi mwenyewe anaitwa Ngũgĩ wa Thiong’o yaani, ni Ngũgĩ mwana wa Thiong’o. Vivyo hivyo, *Gitutu wa Gataanguru* lina maana ya Gitutu mwana wa Gataanguru. Uhusisho huu wa mwana na baba unadhihirika katika majina ya wezi wote wanaorejelewa. Kwa mfano; *Kihaahu wa Gatheeca* ambaye jina lake ni la kimajazi. Taswira tunayochorewa na maelezo ya mwandishi ni kwamba muhusika huyu ni mrefu na mwembamba. Sifa hii inahusiana moja kwa moja na jina la baba *Gatheeca* ambalo linaweza kuhusishwa na kitenzi *Gutheeca* chenye maana ya kudunga. Jina lake *Kihaahu* limetokana na kitenzi *Hahura* chenye maana ya kutia wasiwasi. Maelezo yake katika kutoa ushuhuda wa jinsi alivyo bingwa wa wizi ni dhihirisho tosha. Kwa mfano, anajieleza ifuatavyo:

*Ni nii nderi iria ireraga riera-ini huungu ikoorira itara-ini*

Hii ina maana ya

*Mimi ndiye tai ambaye humfanya mwewe kukimbilia kiotani.*

Tukiangazia kifungu hiki, Kihahu wa Gatheeca anajifaninisha na tai ambaye ni mkali kiasi cha kumtia mwewe wasiwasi na kumfanya kukimbia na kujificha. Kwingineko, Kihaahu wa Gatheeca anajidai kuwa anapenda kushiriki mapenzi haramu na wake za watu kiasi cha kuwafanya waachane na waume zao. Majazi yanatokea katika hali ya kumithilisha kitendo cha ngono na kitendo cha kudunga kama jina lake la pili linavyoashiria.

*Mwireri wa Mukirai* naye ni mmoja wa wezi wanaoshindana pale pangoni. Hata hivyo ushuhuda wake hauwaridhishi walioko pale kwa kuwa “hajafikia kiwango” kilichowekwa na watangulizi wake kuhusu mali waliyonayo. Anawatuliza kwa kuwaambia kuwa: *Nguuguni iireagira ruku-ini na ikaaya kuigana* kwa maana ya kunguni hujitunza akiwa kwenye ukuni hadi akawa mkubwa. *Mwireri wa Mukirai* anajitokeza kama muhusika ambaye anaamini katika kujiimarisha; *kwirera-kujilea*, katika wizi kwa kutegemea itikadi.

*Nditika wa Nguunji* naye amepewa jina la kimajazi linaloana na tabia zake. Jina lake linatokana na maneno mawili ya Wakikuyu *Tindika* – kitenzi chenye maana ya kusukuma na

*Kuunja* – kitenzi chenye maana ya kunja. Ushahidi wake unaashiria jinsi anavyowanyanyasa wafanyakazi wake na kutumia uwezo wake kupata chochote atakacho. Unyanyasaji huu unawasukuma wafanyakazi wake kuwa masikini zaidi. Aidha anaamini katika unyakuzi wa mali ya umma kama anavyoeleza mwenyewe katika ushuhuda wake (Matini chanzi ukurasa wa 178)

Rekeei andu aitu turiganirwo ni mauundu maathirire. Icio ciari irooto  
njuru...mahahura-toro. Rekeei riu tugwatanire mauundu matatu: *kuhuria*,  
*Gukuunja na Gutitika*. Utatu Mutheru. *Huria Kuunja, Titika* uroreetie na gwaku.  
(Msisitizo wangu)

Maneno yaliyo katika herufi za mlazo yana maana ya *Kunyakua, Kukunja na Kubeba*. Anarejelea hali hizi tatu kuwa utatu mtakatifu wa wizi wa kisasa. Maneno haya yanaoana na jina alilopewa na kwa jinsi hiyo jina lake ni la kimajazi.

Tukiangazia jinsi majina haya ya kimajazi yameshughulikiwa katika tafsiri ya Kiingereza, tunapata kwamba majina yamedumishwa jinsi yalivyo katika matini chanzi. Shirinzadeh na Mahadi (2014) wanaeleza kwamba katika kutafsiri nomino za pekee kama vile majina ya wahusika, mielekeo miwili inayopendelewa sana ni ule wa uhawilishaji wa jina jinsi lilivyo kutoka lugha chanzi na ule wa kulitafsiri jina husika kuafiki mfumo wa lugha pokezi. Mtafsiri katika muktadha huu alidumisha majina haya jinsi yalivyotumiwa katika matini chanzi. Huenda hali hii ilichangiwa pakubwa na ukweli kwamba majina haya ni ya kubuni; hayapo katika utamaduni halisi wa jamii ya Wakikuyu, isipokuwa jina Mwaura na Robin. Isitoshe, uamuzi wa kuyadumisha jinsi yalivyo huenda ulichangiwa na haja ya kuwasilisha majazi ambayo hayangeumbika upya katika mifumo ya matini tafsiri. Uamuzi huu hivyo basi unaishia kuibua ugeni katika matini hizi na kuashiria kwamba si matini asilia katika mfumo wa Kiingereza.

### Hitimisho

Matukio ya uibuaji wa ugeni katika mifumo ya lugha za kigeni yanayotokana na tafsiri sisisi katika msingi wa baadaukoloni ni ya lazima kutokana na haja ya kueleza tajriba za kiasili na tamaduni asili katika uandishi wa Kiafrika. Hii ni njia ya kipekee ya kuzipa lugha na tamaduni hizi za kiasili mchomozo na kuziwezesha katika mazingira jirani na lugha za kipebari ambazo awali ziliangaziwa kuwa zenye uwezo na mamlaka zaidi. Isitoshe, ni kweli kwamba, uibuaji ugeni ni mkakati ambao unahusishwa na jududi za upinzani wa namna yake ambapo, katika mfano wa matini tulizoshughulikia, tafsiri za uibuaji ugeni zinakuwa jukwaa la mapambano ya lugha na tamaduni za kiasili dhidi ya lugha na tamaduni babe za kikoloni kwa lengo la kuzikomboa na kuziwezesha. Upinzani huu ni wa kimsingi kwa kuwa unapanua mawanda ya tamaduni na lugha ambazo zilitweza huku tafsiri hizi zikitia doa katika lugha na tamaduni za kibepari ambazo awali zilikuwa zimetukuzwa. Kutokana na uchanganuzi wetu, uibuaji ugeni umeweza kuhusishwa na vipengele vitatu vikuu ambavyo ni; kwanza, lengo la tafsiri yenyewe pamoja na hadhira inayolengwa, pili ni uamuzi wa mtafsiri mwenyewe ambao unaathiriwa na mtazamo na msimamo wake, na mwisho ni tofauti za kiisimu na za kitamaduni baina ya mifumo inayohusika katika tafsiri jambo ambalo linasababisha kukosekana kwa visawe kamili. Ingawa hivyo, katika mazingira ya baadaukoloni, uibuaji ugeni pakubwa ni tukio la kimakusudi ambalo tunalihusisha na hali mbili za kwanza. Kwa kuhitimisha, mtafsiri amebainishwa kuwa kiungo

muhimu katika mchakato wowote wa tafsiri. Mtazamo wa tafsiri nzuri kama gae la kioo ambalo halionyeshi tofauti baina ya mtu na sura yake isipokuwa pale palipo na kasoro hauna mashiko. Mtafsiri anatekeleza jukumu muhimu katika tafsiri. Maamuzi anayofanya, ama kwa makusudi au hata kwa kutokusudia huathiri sio tu mchakato wenyewe wa tafsiri bali pia zao la tafsiri. Kwa jinsi hii, udhihirikaji wa mtafsiri ni kipengele cha kimsingi katika taaluma ya tafsiri iwe ni katika kutalii maadili au hata katika kuhakiki matini tafsiri.

**Marejeleo**

- Alvarez, R. & Vidal, C. (1996). *Translation, Power, Subversion*. Clevedon/Philadelphia: Multilingual Matters.
- Baker, M. (1992). *In Other Words: a coursebook on translation*. London: Routledge.
- Bandia, P. F. (2008). *Translation as Reparation: Writing and Translation in Postcolonial Africa*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Bandia, P. F. (2010). "Postcolonial Literatures and Translation." In: Gambier, Y & Doorslaer, L (Eds). *Handbook of Translation Studies*. (Vol. 1)
- Bandia, P. F. (2014). *Translation as Reparation: Writing and Translation in Postcolonial Africa*. New York: Routledge.
- Catford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. Oxford: Oxford University Press.
- Cook, D. & Okenimkpe, M. (1997). *Ngũgĩ: An Exploration of His Writings*. (2<sup>nd</sup> Ed). New Hampshire: Heinemann
- Cronin, M. (2003). *Translation and globalization*. London: Routledge.
- Cronin, M. (2006). *Translation and identity*. London: Routledge.
- Holmes, J. (1972): *The Name and Nature of Translation Studies*, unpublished manuscript, Amsterdam, Translation Studies section, Department of General Studies, reprinted in Toury, G. (ed.) (1987): *Translation Across Cultures*, New Delhi, Bahri Publications.
- Marais, K (2018) *A (Bio)Semiotic Theory of Translation: The Emergence of Social-Cultural Reality*. London/New York: Routledge.
- Marais, K (2014) *Translation Theory and Development Studies: A Complexity Theory Approach*. London/New York: Routledge.
- Nida, E. A. (1964). *Towards a Science of Translating: With Special Reference to Principles and Procedures Involved in Bible Translating*. Leiden: Brill.
- Ngugi, T. (1986). *Decolonizing the Mind: The politics of Language in African literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Ngugi, T. (1981). *Detained: A writer's prison diary*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Nord, C. (1990). Functionalism and loyalty: some considerations around the translation of titles. *Proceedings of the II Complutense Meetings on Translation*, 153-162.
- Reiss, K na Vermeer, J (1984). *Towards a General Theory of Translational Action Skopos Theory Explained*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Shirinzadeh, S.A & Mahadi T.S (2014). "Translating Proper Nouns: A Case study of English Translation of Hafez's Lyrics. In. *English Language Teaching*, 7(7). Canadian Centre of Science and Education.
- Snell-Hornby, M (2006). *The turns of translation studies. New paradigms or shifting viewpoints?* Amsterdam: John Benjamins.
- Toury, G (1995). *Descriptive Translation Studies and Beyond*. Amsterdam / Philadelphia: John Benjamins Publishing Company
- Tymoczko, M. and Gentzler, E. (2002). *Translation and power*. Amherst: University of Massachusetts Press.
- Venuti, L. (1995). *The Translator's Invisibility: A History of Translation*. London & New York: Routledge.